**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA SABA

**11 MEI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA SABA – TAREHE 11 MEI, 2016

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

## II. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 140. MHESHIMIWA MGUMBA TEBWETA OMARY (MOROGORO KUSINI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Sera ya Serikali ni kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya vijana na kinamama kwa mujibu wa sheria ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu; lakini Halmashauri nyingi ikiwemo ya Morogoro Vijijini haitoi mikopo hiyo kwa makundi hayo kama ilivyokusudiwa:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuzibana na kuziamuru Halmashauri zote ikiwemo Halmashauri ya Morogoro Vijijini kutenga 5% ya fedha za mapato ya ndani kwa vijana na 5% kwa ajili ya kinamama ili waweze kupata mikopo yenye riba nafuu na kutimiza lengo lililokusudiwa.

**141. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kituo cha Afya cha Kirando katika Wilaya ya Nkasi kinatoa huduma kwa vijiji zaidi ya ishirini katika Mwambao wa Ziwa Tanganyika na katika Kituo hicho wodi za watoto na kinamama zimekuwa ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya watoto na kinamama wanaohudumiwa katika kituo hicho:-

Je, ni lini Serikali itajenga wodi hizo ili kuondoa kero kwa kinamama na watoto wanaohudumiwa katika kituo hicho.

**142. MHESHIMIWA SIKUDHANI YASINI CHIKAMBO (VITI MAALUMU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Tunduru inayohudumia Majimbo mawili ina tatizo la gari la kubebea wagonjwa ambapo gari lililopo ni moja na linaharibika mara kwa mara:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari jipya katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru.

**143. MHESHIMIWA KANYASU CONSTANTINE JOHN (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Shule ya Sekondari ya Wasichana Nyankumbo ilijengwa na mradi wa GGM kusaidia kundi kubwa la wasichana wasome Wilayani Geita, shule hii ina hosteli za kutosha na nyumba za walimu:-

Je, ni kwa nini shule hiyo imebaki kuwa shule ya kutwa wakati mazingira yake yanafaa kuwa sekondari ya Bweni.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

**144. MHESHIMIWA PASCAL YOHANA HAONGA (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Shirika la NAFCO Magamba limeshindwa kuyaendesha mashamba yaliyochukuliwa kutoka kwa Wananchi na kuwakosesha maeneo ya kulima na mara nyingine kuwakodishia kwa gharama kubwa:-

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kuyarejesha mashamba hayo kwa Wananchi.

**145. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA: (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Moja ya njia ya kuimarisha uchumi ni kupunguza uagizaji wa bidhaa nje ya nchi; Taifa linatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza mafuta ya kula wakati kuna vyanzo vingi vya mafuta kama vile Alizeti - Singida na Michikichi - Kigoma:-

Je, ni lini Serikali itaweka msukumo kwa mazao haya katika Mikoa hii kwa faida ya nchi na wakazi wa Mikoa hiyo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**146. MHESHIMIWA MATTAR ALI SALUM (SHAURIMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Makazi ya Maaskari yamekuwa ya zamani pia mengine yamekuwa mabovu sana mfano nyumba za Ziwani Zanzibar, Wete, Pemba na Chakechake Pemba hazikaliki kabisa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia marekebisho nyumba hizo;

(b) Je, ni gharama gani Serikali itatumia kwa marekebisho ya nyumba hizo.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

### 147. MHESHIMIWA OSCAR RWEGASIRA MUKASA (BIHARAMULO MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Wananchi wa Kijiji cha Busiri Wilayani Biharamulo ni miongoni mwa Watanzania wanaoendesha maisha yao kwa shughuli za uchimbaji mdogomdogo ambazo zinahitaji kuungwa mkono na Serikali kimkakati:-

a) Je; Serikali ina mkakati gani wa kuwaunga mkono wachimbaji wadogowadogo wa Busiri;

b) Je; Serikali iko tayari kuwatembelea wananchi wa Busiri na kuwaelewesha ni namna gani na ni lini itaanza kutekeleza mkakati huo wa kuwaunga mkono wachimbaji wadogowadogo.

### 148. MHESHIMIWA MUSUKUMA JOSEPH KASHEKU (GEITA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Mkandarasi wa REA anayefunga umeme katika Jimbo la Geita Vijijini amemaliza tatizo ni yule anayeunganisha kutoka Sengerema yuko polepole sana:-

Je, ni lini sasa Serikali itamsimamia kikamilifu mkandarasi huyo ili aweze kumaliza kazi hiyo na umeme uweze kuwashwa.

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**149. MHESHIMIWA SAVELINA SILVANUS MWIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Viwanda vingi hapa nchini vimekuwa vya kizamani, vingine vimetelekezwa na wawekezaji na baadhi hufanya kazi kwa kusuasua hasa katika Mkoa wa Kagera:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuviboresha viwanda hivyo ili viweze kufanya kazi vizuri kwa faida ya nchi yetu.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

**DODOMA**
**11 MEI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**